BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 24 Juni, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar:**

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora ndani yake.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti bora ndani yake.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

279. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika kifungu cha 132 (b) cha Ilani ya CCM, kwenye mambo mtambuka ya kidiplomasia, Serikali ilielekezwa kuzihamasisha Balozi na Jumuiya za Kimataifa kufungua ofisi ndogo za uwakilishi hapa Zanzibar.

Je, tokea 2020 hadi sasa, ni mafanikio gani yamepatikana katika jambo hilo.

## Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

269. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ni tegemeo kubwa sana katika jamii ya Waislamu wa Zanzibar. Hata hivyo, changamoto ya upatikanaji wa fedha inaweza kuwa kikwazo cha Kamisheni hii kukidhi mategemeo ya Waislamu hao.

(a) Je, kwa wastani, ni kiasi gani cha mapato hupatikana kila mwezi kutokana na mali za wakfu.

(b) Je, kwa kawaida, fedha zinazotokana na mali ya wakfu hutumika katika shughuli gani.

(c) Je, ni kwa kiasi gani fedha hizi hutumika kuimarisha misikiti, madrasa na nyumba za kulelea watoto mayatima.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

221. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni maeneo gani stahiki yanaruhusika kwa ajili ya maegesho ya magari “Parking” na maeneo gani hayaruhusiki kuweka “Parking” ndani ya mji wa Zanzibar.

## Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

129. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na malalamiko mengi kwa wafanyabishara wanaoingiza mizigo yao Zanzibar kutokea Tanzania bara na nchi jirani, wakilalamikia utitiri wa kodi pale mizigo yao inapofika bandarini. Hali hii hutokana na mfanyabishara kutakiwa kulipa ushuru kwa taasisi mbali mbali za Serikali, hali

inayoleta usumbufu mkubwa kwa wafanyabiashara hao.

(a) Je, ni lini Serikali itaunganisha mifumo yake na kuyafanya malipo yote kulipwa mara moja na taasisi kugawana malipo hayo kupitia mfumo husika.

(b) Je, ni malipo ya namna gani ambayo mfanyabiashara hutakiwa kulipa anapoingiza mizigo yake bandarini Zanzibar.

(c) Je, ni mapato ya kiasi gani Serikali hupata kwa mwaka kwa wafanyabiashara wanaoingiza mizigo yao bandarini Zanzibar kutokea Tanzania bara na nchi jirani.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

237. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya lugha ya Kiswahili kupitia mitandao mbali mbali ya kijamii.

(a) Je, Wizara yako inasimamia vipi upotoshaji mkubwa unaofanyika wa matumizi ya kimsamiati sanifu na fasaha katika kuilinda lugha yetu ya Kiswahili.

(b) Nani anabeba jukumu la kukiweka sawa kiusanifu na kiufasaha Kiswahili kinachotumika kwenye tafsiri za mitandao mikubwa ya kijamii kama vile GOOGLE na mengineyo.

**Wizara ya Afya:**

21. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha Afya cha Shakani kinakabiliwa na changamoto tofauti zikiwemo uchakavu wa jengo, uchache wa vitendea kazi na kutokuwepo kwa miundombinu rafiki inayoendana na mahitaji ya vituo vya afya vya kisasa. Katika kuwapa matumaini wananchi wetu, viongozi mbali mbali wa Serikali waliwahi kutoa ahadi tofauti juu ya kuziondoa changamoto hizo, lakini hadi leo bado ahadi hizo hazijatekelezwa.

Je, ni lini Wizara yako itatekeleza ahadi za viongozi ili kuziondosha changamoto hizo.

81. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hospitali ya Kivunge inakabiliwa na ukosefu wa nyumba za wafanyakazi, ambapo asilimia 80 ya wafanyakazi wake wanaishi mbali na hospitali katika mkaazi yao binafsi, huku nyumba za makaazi za wafanyakazi hao zilizopo karibu na hospitali hiyo ni chakavu na za zamani.

(a) Kwa kiwango gani Wizara yako inalifahamu suala hili.

(b) Je, Wizara yako inachukuwa hatua zipi kulitatua tatizo hili.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

46. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kurekebisha mitaala yake ya elimu na msisitizo pia umewekwa kwa Elimu ya Amali.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuwaandaa walimu na wataalamu katika kufundisha masomo ya amali, ili kwenda sambamba na mtaala mpya.

(b) Je, ni mara ngapi kwa mwaka Wizara yako inafanya tathmini ya ubora wa elimu ili kwenda sambamba na marekebisho ya mitaala mipya kwa namna itakavyohitajika.

263. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hivi karibuni kupitia mitandao ya kijamii ilionekana ‘clip’ ya maji chumvi toka baharini yanazunguka eneo la skuli ya Sekondari ya Haile Salasie, hali iliyoleta mfadhaiko kwa watu wengi.

(a) Je, jambo hili ni la kweli au ni mambo ya mitandao tu.

(b) Kama ni kweli ni sababu gani za msingi zilizopelekea jambo hilo na ni hatua gani za dharura zilizochukuliwa na Serikali kukabiliana nalo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

152. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali imeibinafsisha bandari ya Malindi Unguja kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kiutendaji wa kila siku hapo bandarini.

(a) Je, ni kwa kiasi gani lengo na dhamira iliyokusudiwa imekamilika.

(b) Je, ni ipi tofauti ya kiutendaji ya utoaji wa makontena hapo zamani na sasa.

(c) Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi juu ya mtazamo wao wa kiutendaji kwa kampuni iliyobinafsishiwa bandari hiyo.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:**

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti bora ndani yake – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**24 Juni, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**